1/11/2022

TOLEO LA 16.

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA

# GAZETI

# WAZIRI MAKAMBA AZINDUA BODI YA TPDC



**Arusha, Tanzania**

Mnamo tarehe 20 Mei 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** alimteua Balozi Ombeni Sefue kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania **(TPDC)**...

UK. 1

## TPDC YACHANGIA SHILINGI MILIONI 100 JKCI

UK. 8

## TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA AFRICA OIL WEEK

UK. 12

## MKURUGENZI MTENDAJI WA TPDC ATEMBELEA MAONESHO YA SABASABA

UK. 2



## NYUMBA 570 ZAUNGANISHWA MTANDAO WA GESI ASILIA DSM

UK. 3

# BODI YA WAHARIRI

**MHARIRI MKUU**

Marie Msellemu

**WAJUMBE**

Malik Munis
Beatrice Peter
Oscar Mwakasege
Delian Kabwogi
Ally Mluge
Kwigema Anthony
Eugene Isaya
Jacobo Haule

## LIMETOLEWA NA:

Kitengo cha Mawasiliano
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
Benjamin W. Mkapa Pensions
Towers, Azikiwe/Jamuhuri Street
S.L.P. 2774, Dar Es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2200103/4, 2200112.
Nukushi: +255 22 22 2200113
Barua pepe: info@tpdc.co.tz
Tovuti: www.tpdc.co.tz

## TAHARIRI

# Gesi Asilia Kukuza Uchumi Wa Nchi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) imekuwa mstari wa mbele katika kufanya tafiti mbalimbali za mafuta na gesi asilia Nchini. Tafiti hizo zimezaa matunda mpaka gesi asilia ikagunduliwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

**Mwaka 2004** nchi yetu ilianza kutumia gesi asilia kwa mara ya kwanza kupitia gesi iliyogunduliwa Mkoani Lindi (Kisiwa cha Songosongo).

**Mwaka 2007** gesi asilia ilianza kutumika Mkoani Mtwara na hata katika matumizi ya umeme ulianza kuzalishwa kwa kutumia gesi asilia.

**Mwaka 2011** Serikali iliona ni vyema kutanua wigo wa matumizi ya gesi asilia ili iweze kuleta manufaa katika matumizi mbalimbali.

**Mwaka 2015** Mradi wa bomba la gesi asilia na Mitambo ya kuchakata gesi ya Madimba (Mtwara) na Songosongo (Lindi) ilianza rasmi, hivyo tangu hapo gesi asilia ilianza kutumika kuzalisha umeme, kutumika viwandani, kutumika kwenye magari na majumbani.

Kama mnavyojua matumizi ya nishati yanaongezeka kila siku na watumiaji wanaongezeka, Serikali imeona umuhimu wa kuendelea kutumia vyanzo vyote ambavyo gesi inapatikana.

Eneo la Ntorya katika Kata ya Nanguruwe Mkoani Mtwara ni moja ya eneo ambalo tayari ugunduzi wa gesi ulishafanyika tangu mwaka 2011 hivyo Serikali inahitaji iitumie gesi hiyo, iweze kupelekwa kwenye Kiwanda cha kuchakata gesi cha Madimba ili iweze kuwa na mchango katika kuongeza matumizi ya gesi asilia.

Hivyo, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa kilomita 35 ambalo litajengwa kwa takribani Shilingi **Bilioni 70** ambapo utekelezaji wa mradi huo umeshaanza na kwa sasa zoezi linalofanyika ni la uthamini wa ardhi, mashamba, mazao na mali zingine za wananchi wa vijiji 13 (Namayakata Barabarani, Ngorongoro, Mwindi, Mbawala, Mduwi, MailiKumi, Nachenjele, Lukweta, Minyembe, Ding'wida, Namindodi,Mtendachi na Msakala) watakaopisha mkuza wa bomba hilo kutoka Ntorya hadi Madimba.

# WAZIRI MAKAMBA AZINDUA BODI YA TPDC



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

**Arusha,**

Mnamo tarehe 20 Mei 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alimteua Balozi Ombeni Sefue kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Kufuatia uteuzi huo mnamo tarehe 10 Juni 2022 Waziri wa Nishati, Mhe. January Y. Makamba (Mb) aliteua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC ili kukamilisha safu ya bodi kwa mujibu wa sheria.

Kufuatia uteuzi huo, mnamo tarehe 4 Julai 2022 Waziri Makamba alizindua rasmi Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC kuashiria kuwakabidhi majukumu yao rasmi katika kuliongoza Shirika la TPDC. Akiongea wakati wa uzinduzi wa Bodi hiyo, Waziri Makamba alisema "TPDC ni miongoni mwa Mashirika ya Umma ya awali kabisa kuundwa baada ya kupata uhuru, hii ni kutokana na umuhimu wa Taifa kuwa na Shirika la Taifa la Mafuta na umuhimu wake umeendelea kuonekana hadi leo hii ambapo tuna ugunduzi wa futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia na shughuli za utafutaji wa mafuta zinaendelea sehemu mbalimbali katika nchi yetu".

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, Balozi Ombeni Sefue alisema "Tuna majukumu makubwa mbele yetu lakini niseme tu kuwa mimi ninaamini katika kufanya kazi kama timu yenye malengo ya pamoja na kwa utaratibu huo nina imani kuwa tutafika mbali na kutimiza ndoto za Rais wetu za kufunga magoli mengi (kupata mafanikio zaidi)".

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alisema "Siku ya leo ni kubwa na ya muhimu sana kwetu TPDC, tumekuwa tukijiendesha kwa kipindi cha miaka mitatu bila bodi baada ya bodi iliyokuwepo kumaliza muda wake hivyo leo tunavyozindua bodi mpya tunajiskia faraja kama Taasisi". Dkt. Mataragio alifafanua zaidi kwa kueleza kuwa TPDC imepata Bodi mahiri yenye watu wazoefu kwenye sekta ya mafuta na gesi na wabobezi katika uwekezaji na utendaji wa sekta binafsi.

# MKURUGENZI MTENDAJI WA TPDC ATEMBELEA MAONESHO YA SABASABA

**Dar es Salaam,**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio tarehe 07/07/2022 alitembelea Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) katika banda la TPDC Jijini Dar es salaam.

Akizungumza na Waandishi wa Habari katika banda hilo Dkt. Mataragio alisema kuwa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa mpaka sasa ni futi za ujazo Trilioni 57.54 tcf. "Kiasi hiki cha gesi asilia kimeendelea kuwa msaada mkubwa kwa Watanzania kutokana na matumizi yake kufikia asilimia 62 huku kiasi kikubwa cha gesi kikiwa baharini".

Alisema kiasi kikubwa cha gesi ambacho kipo baharini kinatarajiwa kuvunwa kupitia mtambo wa kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) unaotarajiwa kujengwa eneo la Likon'go Mkoani Lindi ambapo gesi itakayopatikana itasafirishwa kwenda kuuzwa kwenye masoko ya nje ya nchi na nyingine kubaki nchini kwa ajili ya soko la ndani.

Aidha, Dkt. Mataragio aliwaomba Watanzania kutumia fursa hiyo kwa kuanzisha Makampuni yanayotumia gesi asilia ili waweze kunufaika zaidi na fursa hiyo, pia kwa kutumia gesi asilia watakuwa wameshiriki kuokoa uharibifu wa mazingira.



**Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio (mwenye koti la bluu) alitembelea Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa na kuzungumza na baadhi ya Wananchi kuhusu elimu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani kwenye Viwanja vya Maonyesho ya Biashara (Saba Saba) Jijini Dar es salaam.**

# BODI YA TPDC YAANZA KAZI, YAFANYA ZIARA MTWARA NA LINDI

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) inayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Sefue imefanya ziara ya kikazi kutembelea miradi ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara.



Akiongea baada ya kuona kazi za ukusanyaji takwimu za mtetemo kwa mfumo wa 3D katika kitalu cha Ruvuma kinachoendeshwa na ARA Petroleum Tanzania, Balozi Sefue alisema "Matumizi ya gesi asilia hapa nchini yameendelea kukuwa siku baada ya siku hivyo kazi inayofanyika katika kitalu hiki inalenga kuongeza uzalishaji wetu wa gesi asilia ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mahitaji yake".

Balozi Sefue alioneshwa kuridhishwa na kazi zinazoendelea katika kitalu cha Ruvuma na kuwaasa ARA Petroleum Tanzania kuendelea na kasi hiyo ili kuendana na uwekezaji unaofanyika ndani ya nchi ambao kwa kiasi kikubwa unahitaji nishati.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alieleza namna TPDC kama mwenye leseni zote za vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi hapa nchini anavyoshirikiana na wawekezaji katika mkondo wa juu kuhakikisha shughuli za utafutaji na uendelezaji wa rasilimali hizi unaendelea kwa kasi.

Dkt. Mataragio alisema "TPDC kwa kushirikiana na wawekezaji tumeendelea kufanya kazi mbalimbali za kitaalam zenye lengo la kuhakikisha kuwa tunaendeleza sekta yetu ya gesi na mafuta na kuendana na ongezeko la mahitaji ya gesi asilia ndani na nje ya nchi".

Aidha, Meneja Mkuu wa ARA Petroleum Tanzania, Ndg. Erhan Saygi alieleza mategemeo yao kama kampuni ni kuzalisha gesi katika visima vya Ntorya 1, Ntorya 2 pamoja na Chikumbi 1 ambacho kiko katika maandalizi ya awali. "Tumepanga kukamilisha kazi ya ukusanyaji wa takwimu za mtetemo mwezi Novemba na kuanza kuchimba kisima cha Chikumbi 1 ambacho kitakuwa cha tatu katika kitalu hiki mapema mwaka 2023".

Ndg. Erhan pia alieleza mategemeo yao ni kuzalisha futi za ujazo milioni 60 kwa simu (60mmscfd) kwa kuanzia na uzalishaji utaendelea kukuwa kadri mahitaji ya gesi yatakavyokuwa.

# MAKAMBA: NCHI BADO HAIJAGUNDUA MAFUTA, TPDC INAENDELEA NA UTAFITI EYASI WEMBERE

**Simiyu, Tanzania**

Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba alisema Tanzania bado haijagundua mafuta, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) inaendelea na jitihada za utafiti katika Bonde la Eyasi Wembere.

Mhe. Makamba aliyasema hayo alipokuwa akifanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu pamoja na Waandishi wa Habari, tarehe 13 Julai, 2022 Mkoani Simiyu.

"Nchi yetu bado haijagundua mafuta, kumekuwa na jitihada za makusudi zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Shirika la TPDC ili kuhakikisha na sisi tunagundua mafuta. Kwa sasa TPDC ipo katika hatua nzuri ya utafiti wa mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere. Kutokana na matokeo ya kitaalamu, yapo matumaini makubwa kwamba huenda mafuta yakagunduliwa," alisema Makamba.

Mheshimiwa Makamba aliongeza, "Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Serikali na unahusisha Mikoa mitano (5) ambayo ni; Arusha (Wilaya ya Karatu), Singida (Wilaya za Iramba na Mkalama), Simiyu (Wilaya ya Meatu), Shinyanga (Wilaya ya Kishapu) pamoja na Tabora (Wilaya ya Igunga).

Aidha, Meneja wa Mradi wa utafutaji mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere kutoka TPDC, ndugu Sindi Maduhu, alisema, tangu kuanza kwa mradi 2015, kuna baadhi ya hatua ambazo mradi umepitia,hatua hizo zilihusisha shughuli za kisayansi kama vile ukusanyaji wa taarifa za usumaku na uvutano kwa kutumia ndege, kuchoronga mashimo mafupi ya utambuzi wa miamba na kwa sasa Shirika linaendelea na shughuli ya ukusanyaji wa taarifa za kijiokemia zitakazowezesha kutambua uwezekano wa uwepo wa mafuta yanayovuja kutoka ardhini, kwa kutumia teknolojia maalumu ya moduli (Amplified Geochemical Imaging).

Maduhu aliongeza kuwa, "hatua hizi za kisayansi zinatoa matumaini makubwa ya uwepo wa mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere. Hii inatokana na sababu kwamba, taswira za miamba iliyopo Eyasi Wembere inafanana kwa kiasi kikubwa na taswira za miamba ya Ziwa Albert nchini Uganda na Ziwa Turkana nchini Kenya, ambapo tayari mafuta yamegundulika katika sehemu hizo. Hivyo hata sisi tunapoendelea na utafiti tunaamini huenda tukagundua mafuta ambayo yataleta tija katika uchumi wa Taifa.

Kitalu cha Eyasi Wembere kipo Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania ndani ya Bonde la ufa la Afrika Mashariki. Bonde hili linapita katika Mikoa ya Arusha, Singida, Tabora, Shinyanga na Simiyu. Bonde hili ni moja ya maeneo yenye miamba tabaka yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta au gesi asilia. Aidha, eneo hili lipo katika ukanda mmoja na mabonde ya Lokichar (Kenya) na Ziwa Albert (Uganda) ambapo mafuta yamegundulika.

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA AFRICA OIL WEEK

**Cape Town, SA**

Tanzania iliungana na nchini nyingine Afrika katika kushiriki mkutano wa Africa Oil Week uliofanyika katika Jiji la Cape Town nchini Afrika Kusini kwa siku 5 mfululizo kuanzia tarehe 3 hadi 7 Oktoba 2022. Mkutano huo uliwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya mafuta na gesi, ulilenga kujadili kuhusu mabadiliko ya matumizi ya nishati kutoka nishati zenye kutoa hewa ukaa nyingi kuelekea nishati zenye kutoa kiasi kidogo cha hewa ukaa ikiwa ni mikakati ya kidunia kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.




Katika Mkutano huo Tanzania iliwakilishwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato (Mb) ambae pia aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu Balozi Ombeni Sefue pamoja na timu ya wataalam kutoka Wizara ya Nishati, TPDC na PURA. Akiongea katika mkutano huo, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato alisema "Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuchochea matumizi ya gesi asilia ambayo ni nishati safi na salama kwa mazingira ambapo kwa sasa asilimia zaidi ya 60 ya umeme katika gridi ya Taifa unatokana na gesi asilia ambayo imekuwa ni mbadala wa mafuta mazito".

Nae Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, Balozi Ombeni Sefue alieleza ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa Africa Oil Week unatoa nafasi ya kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta ya mafuta na gesi na kuendelea kujitangaza kama nchi yenye mazingira rafiki ya uwekezaji. "Tunashiriki mkutano huu tukiwa na malengo ya kimkakati ya kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta yetu ya mafuta na gesi Tanzania na pia kuonyesha maendeleo ambayo tumeyafikia sisi kama nchi katika kuendeleza rasilimali asilia hususan gesi asilia" alieleza Balozi Sefue. Katika kuhakikisha hili linafanikiwa, TPDC kama Shirika la Taifa la Mafuta limeweka banda la maonesho na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika utafutaji wa mafuta na gesi nchini.

# MRADI WA EACOP NI SALAMA KWA MAZINGIRA



Waziri wa Nishati January Makamba amewatoa hofu watanzania juu ya usalama wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga Tanzania akisema wanaopinga Mradi huo ni wanaharakati wasioitakia mema Tanzania

Waziri Makamba aliyasema hayo wakati akikagua maendeleo ya Ujenzi wa Mradi huo katika Kijiji cha Sojo Wilaya ya Nzega Tabora ambapo patajengwa karakana ya kupaka rangi mabomba yatakayotumika kusafirishia mafuta hayo kutoka Uganda hadi Tanga

Aidha Makamba alisema wakati wa kutafuta maeneo ya kupitishwa Bomba hilo Serikali ilizingatia usalama wa mazingira na usalama wa watanzania huku ikihakikisha Bomba hilo halileti madhara zaidi ya kunufaisha watanzania na Taifa kwa ujumla

Akiongea na Waandishi wa Habari kwenye eneo la Mradi huo Kijiji cha Sojo Makamba aliwataka Wakandarasi kutimiza majukumu yao kwa weledi na kutimiza makubaliano waliyoingia na Serikali ili Mradi huo ukamilike kwa wakati uliokusudiwa.

Makamba alisema Mradi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2025 utazalisha Ajira zaidi ya elfu kumi huku ikitarajiwa kuongeza Pato la Taifa kutokana na usafirishaji wa mafuta hayo kutoka Uganda na kwenda Nchi za nje.

Bomba hilo linatarajiwa kuwa la kipekee baada ya kukamilika kwake litakuwa bomba refu zaidi duniani. Kukamilika kwa  Mradi huo kutagharimu dola Bilioni 5.1 za Kimarekani sawa na shilingi Trilioni 11 za Kitanzania.

# ZAIDI YA ASILIMIA 60 YA UMEME UNAZALISHWA NA GESI ASILIA–MWENYEKITI WA BODI –PURA



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Bwana Khalfan Khalfan alitembelea banda la TPDC katika Maonesho ya 46 ya Biashara jijini Dar es salaam mwezi Julai, 2022 nakutoa pongezi kwa TPDC kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa kwa Taifa katika uzalishaji wa umeme.

''Zaidi ya asilimia 60 ya umeme nchini unazalishwa na gesi asilia hivyo nawapongeza TPDC kwa kuhakikisha umeme unapatikana wa kutosha kwenye Gridi ya Taifa,'' alisema Khalfan.

Akizungumza katika banda hilo, Bwana Khalfan alisema kiasi kikubwa cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini kina manufaa makubwa sana kwa Serikali na wananchi wake kwa ujumla

Aidha, Khalfan ameyaomba Makampuni Binafsi na Wadau wa Sekta ya Nishati kuchangamkia fursa kwenye eneo la uwekezaji wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia ili kuongeza kasi ya usambazaji wa Nishati hiyo ili wananchi wengi zaidi waweze kutumia rasilimali hiyo kwani Serikali peke yake haiwezi kuwafikia kwa muda mfupi.

''Mradi wa usambazaji wa gesi asilia kwa wananchi unahitaji fedha nyingi za ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ikiwa mwananchi anapounganishiwa gesi kwa ajili ya matumizi ile ni huduma na sio biashara''.

Vilevile amewasisitiza wananchi kutumia gesi asilia kwenye magari ili waweze kupunguza gharama za maisha.

Serikali kupitia TPDC mpaka sasa imeunganisha nyumba 1,500 na mtandao wa gesi asilia kwa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es salaam, zaidi ya magari 1,500 yanatuma gesi asilia pamoja na viwanda 48 kwa mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Mtwara.






# NYUMBA 570 ZAUNGANISHWA MTANDAO WA GESI ASILIA DSM

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza gesi asilia ambapo nyumba 570 maeneo ya Sinza na Kota za Polisi Kurasini jijini Dar es Salaam zimeunganishwa katika mtandao wa gesi asilia.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alisema " tumekamilisha mradi huu wa nyumba 570 ambao unaongeza idadi ya watumiaji wa gesi asilia majumbani kufikia zaidi ya 2000". Dkt. Mataragio pia alieleza kuwa miradi ya kusambaza gesi asilia majumbani ni miradi endelevu ambayo kila mwaka TPDC inatenga fedha katika bajeti zake kwa ajili ya kutekeleza miradi ya namna hii na kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23 TPDC imetenga zaidi ya Bilioni 20 kwa ajili ya miradi ya kusambaza gesi asilia majumbani

Kwa upande wake Meneja Mradi kutoka TPDC, Mhandisi Angilindile Marandu alisema mradi huu umegharimu shilingi bilioni 2.14 na umetekelezwa na mkandarasi mzawa. Mhandisi Marandu alifafanua pia kuwa mradi huu ulipaswa kukamilika mapema mwaka huu lakini changamoto za UVIKO-19 ziliathiri mnyororo mzima wa usafirishaji mizigo duniani na hivyo kuathiri na mradi huu kupata vifaa kwa wakati.

Akizungumza baada ya kuanza kutumia gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani, Mkazi wa Sinza Ndg. Walter Swai alisema "hakika gesi hii ni mkombozi, tumetumia uniti 0.4 sawa na shilingi 400 kupika makande badala ya shilingi 3000 za mkaa". Ndg. Swai alieleza pia kuwa ameona gesi asilia ina ufanisi mkubwa katika kupika kwani inapika kwa haraka na ni rafiki kwa mazingira. Nae Bi. Assenga ambaye ni mteja katika Kota za Polisi Kurasini alieleza kuwa anafurahia kutumia gesi asilia kwani inampa unafuu wa gharama, "gesi hii ni nzuri kwani naweza kununua hata ya shilingi 3000 nikatumia tofauti na ile ya mitungi ambayo lazima ulipie mtungi mzima"

# UGUNDUZI WA MAFUTA EYASI WEMBERE UTACHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI

**Arusha**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella alisema endapo Tanzania itafanikiwa kugundua mafuta katika bonde la Eyasi Wembere Wilayani Karatu itakuwa ni hatua kubwa na muhimu itakayosaidia kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mongella aliyasema hayo alipokuwa akiongea na Kikosi kazi cha Maafisa kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) walipofika ofisini kwake kutoa taarifa ya maendeleo ya mradi. "Mmenipa taarifa kwamba, mradi wa utafutaji wa mafuta katika bonde la Eyasi Wembere upo katika hatua nzuri, nina imani kwamba, tukifanikiwa kugundua mafuta katika bonde hili, nchi yetu itapiga hatua kubwa kiuchumi," alisema Mhe. Mongella.

Mhe. Mongella alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kusaini makubaliano ya awali ya utekelezaji wa mradi wa LNG utakaofanyika Mkoani Lindi.

"Tanzania imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwemo gesi asilia ambayo iligundulika katika Mikoa ya Kusini, shabaha ya Rais Samia ni kuhakikisha nchi inapiga hatua kubwa kiuchumi, hasa Taifa linapokuwa na nishati ya kutosha ya mafuta na gesi *asilia,"*alisema Mongella.

Aidha Mongella alisema wao kama Mkoa wa Arusha ambako shughuli hizo za utafiti zinafanyika Wilayani Karatu, wapo tayari kushirikiana na TPDC ili mradi huo uweze kukamilika kwa mafanikio makubwa, kwa maslahi mapana ya Taifa.



Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Karatu Mhe. Dadi Kolimba aliwahakikishia Ushirikiano, Ulinzi na Usalama timu ya Mradi katika kipindi chote cha shughuli husika.

"Napenda kuwahakikishia kwamba, Wilaya itatoa ushirikiano wa dhati ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli iliyopo mbele yenu," alisema Mhe.Kolimba.

Awali, akitoa maelezo ya utangulizi kuhusu mradi, Meneja Mradi kutoka TPDC ndugu Sindi Maduhu alisema mradi wa utafutaji mafuta katika bonde la Eyasi Wembere umepiga hatua kubwa na hatua iliyofikiwa hivi sasa ni ukusanyaji wa sampuli za kijiokemia zitakazosaidia kupata taarifa za viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi katika eneo husika.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Shirika limepanga kufanya utafiti wa kijiokemia (Surface Geochemical Survey) wenye lengo la kukusanya taarifa za viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini.Maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya utafiti huo yanahusisha Mikoa mitano (5) ambayo ni Arusha (Karatu), Singida (Iramba na Mkalama), Tabora (Igunga), Shinyanga (Kishapu) na Simiyu (Meatu).




# TPDC YAWAALIKA WATANZANIA KUCHANGIA MATIBABU YA WAGONJWA WA MOYO

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limewaomba watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki mbio za hisani maarufu kama TPDC MARATHON zilizoandaliwa na Shirika hilo kwa lengo la kupata fedha za kusaidia upasuaji kwa watoto 50 wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) Jijini Dar es Salaam.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa (TPDC) Dkt. James Mataragio wakati akizungumza na Waandishi wa Habari kwenye uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha Wananchi kushiriki katika mbio hizo ambapo amesemea TPDC imeamua kuandaa mbio hizo ili kuwasaidia watanzania na kueleza kuwa mbio hizo zitakuwa endelevu kila mwaka.

Aidha amewashukuru Wafanyakazi wa TPDC na washiriki wengine walioandaa TPDC Marathon akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Prof. Mohamed Janabi ambaye alisema kuwa kila mwaka asilimia 1% ya watoto 2,000,000 wanaozaliwa nchini Tanzania sawa na watoto 20,000 huzaliwa na matatizo ya moyo na kati yao asilimia 25% sawa na watoto 5,000 wanafanyiwa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Jakaya Kikwete.

Prof. Janabi aliongeza kuwa kuna watoto 511 wanaosubiri upasuaji hospitalini hapo huku akiahidi kuwa watahakikisha fedha zitakazopatikana zitatumika kikamilifu kwa malengo yaliyokusudiwa na kuongeza kuwa siku hiyo kutakuwa na upimaji wa magonjwa ya moyo bure, utoaji wa chanjo ya Uviko-19 na uchangiaji wa damu kwa hiyari.

Sanjari na hayo Mratibu wa mbio hizo Fred Kwezi aliwahakikishia washiriki wa mbio hizo kuwa kutakuwepo na huduma zote za kimichezo, kiusalama na kiafya na kuwa usajili unafanyika kupitia TPDC pamoja na Waratibu wa mbio hizo ambao ni Goba Road Runners (GRR).

Mbio hizo zenye kauli mbiu isemayo "Kimbia Kwa Afya Yako" zinatarajia kufanyika Septemba 11 mwaka huu katika viwanja vya Farasi Oysterbay Jijini Dar es salaam huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais Mstaafu wa awamu ya nne Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete.



# TANZANIA NA OMAN KUSHIRIKIANA KUKUZA SEKTA YA NISHATI



**Dar es salaam,**

Waziri wa Nishati Mhe.January Makamba amekutana na Mhe. Balozi wa Oman nchini Tanzania Mhe. Saud Hilal Al Shidhani na kuzungumzia fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi hususani katika miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini.

Mazungumzo hayo yamefanyika katika ofisi ndogo ya Wizara ya Nishati Jijini Dar es salaam leo tarehe 16 Agosti,2022 na yalijikita katika kuzungumzia makubaliano mbalimbali yaliyofikiwa wakati wa ziara ya Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan yaliyofanyika nchini Oman Juni, 2022 ambayo aliambatana na Mhe. Makamba na Waziri wa Utalii na Maliasili Dkt. Pindi Chana.

Kupitia Mazungumzo hayo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) litashirikiana na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Oman (OQ) kufanya biashara ya mafuta ya jumla (fuel supply), kujenga vituo vikubwa vya gesi za mitungi (LPG) na kushirikiana na Kampuni Tanzu ya TPDC (TANOIL) ili kufanya biashara ya rejareja ya mafuta.

Halikadhalika, wataalamu kutoka nchini Oman kuendelea kuja nchini Tanzania kuangalia miundombinu ya Bandari na kutazama maeneo ya kuwekeza kwenye miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari na Ghala za dhamana ya forodha pamoja na kubadilishana uzoefu na Tanzania.

Waziri wa Makamba wakati wa mazungumzo hayo amesema Tanzania inatafuta Washirika wa kimkakati ambao watashirikiana na TPDC katika kutafuta mafuta na gesi katika vitalu vilivyopo ili kuchochea ukuaji wa viwanda na kuongeza ukuaji wa uchumi nchini hususan katika miradi ya kimkakati ukiwemo wa Mwalimu Julius Nyerere.

Akizungumza katika Mkutano huo Mhe. Balozi Saud Hilal Al Shidhani pamoja na kutoa salaam za Rais wa Oman amemshukuru Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa utayari wake wa kushirikiana na Oman katika kuendeleza sekta ya nishati.

Aidha, amesema Oman ina ujuzi mkubwa katika masuala ya mafuta hivyo amemhakikishia Waziri Makamba kuwa watashirikiana vyema katika kukuza sekta hiyo nchini Tanzania.

# TPDC YACHANGIA SHILINGI MILIONI 100 JKCI




Rais mstaafu wa awamu ya nne Dkt.Jakaya Kikwete amezitaka Taasisi na Mashirika kuendelea kuchangia fedha pamoja na kuandaa hafla na mashindano mbalimbali yakiwemo ya mbio za hisani (MARATHON) ili kusaidia huduma za matibabu kwa wananchi.

Alisema hayo Jijini Dar es salaam kwenye mashindano ya mbio za hisani yaliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa lengo la kuchangia shilingi milioni 100 kwa ajili ya upasuaji kwa watoto 50 wenye magonjwa ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)

Alisema pamoja na jitihada za Serikali kufanikiwa kujenga na kuweka mashine za kisasa JKCI zenye gharama ya zaidi ya shilingi bilioni tano (5) kufanikisha upasuaji huo kuna Gharama kubwa ambazo Wananchi wa kawaida hawawezi kumudu hivyo kuwepo mashindano kama hayo yataokoa maisha ya watoto wengi walioshindwa kumudu gharama za matibabu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Dkt. James Mataragio alisema, pamoja na majukumu yao mengine waliyonayo kurudisha kwa jamii fadhila ni jambo muhimu kwao hivyo walianzisha mbio hizo kwa lengo la kuokoa maisha ya watoto wenye matatizo ya moyo ambapo mtoto mmoja hutibiwa kwa Sh.15 milioni.

Aidha Dkt.Mataragio alisema kumekuwepo na mwitikio mkubwa wa makampuni na watu binafsi katika kushiriki katika mashindano hayo na kwamba anatamani kuona TPDC Marathon inakuwa zaidi katika misimu mingine kwa kuongeza washiriki na hivyo kukusanya Fedha nyingi zaidi za kuwasaidia Watoto wengi wenye matatizo ya moyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI Profesa Mohammed Janabi alisema kila mwaka watoto milioni mbili wanazaliwa nchini ambapo kati ya hao asilimia 0.8 mpaka moja wana shida ya moyo na kati yao asilimia 25 wanahitaji upasuaji.

Watoto 511 wanasubiria kupewa huduma ya matibabu ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), hivyo kuna kila sababu ya kuwachangia ili kuokoa maisha yao.



# UJENZI WA KIWANDA CHA KUFUNIKA MABOMBA SOJO WAFIKIA 60%

**Tabora,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeridhishwa na kasi ya ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleni Tanga ambapo kazi za awali za ujenzi wa Kiwanda cha kufunika mabomba zimefikia asilimia 60%.

Kutokana na kasi ya ujenzi huo TPDC imefurahishwa zaidi kuona fursa mbalimbali za ajira zikitolewa kwa wananchi wazawa wanaozunguka mradi huo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo Dkt. James Mataragio baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo na kujionea shughuli mbalimbali za ujenzi wa Kiwanda cha kufunika Mabomba (Themo Isolation) katika Kijiji cha Sojo, Kata ya Igusule, Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora.

Dkt. Mataragio alifanya ziara hiyo Septemba 15,2022 na kumtembelea mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Bwana Kazimila Patrick Mshandete ambaye alikubali kutoa eneo lake kwa ajili ya kupisha mradi huo na Serikali imemlipa fidia na kumjengea nyumba ya kisasa na kuendelea kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula kila mwezi.

“Nimefurahi kuona kazi ya ujenzi wa mradi inaendelea vizuri na wazawa zaidi ya 180 wamepata ajira katika kazi hizi za awali" alisema Dk. Mataragio.

Aidha Dkt. Mataragio alisema Serikali ilisaini Mkataba wa Msingi wa Mradi (Host Government Agreement (HGA) kati yake na Mwekezaji, Kampuni ya EACOP ambapo, kupitia Mkataba huo umeainisha baadhi ya huduma na bidhaa zitakazotolewa na Watanzania pekee ikiwemo huduma za usafirishaji, ulinzi, chakula na vinywaji, huduma za malazi na usambazaji wa mafuta kwa ajili ya magari na mitambo.

Hivyo alisema anafurahi kuona Makampuni ikiwemo Vodacom kujenga mnara wa mawasiliano katika eneo hilo huku akiomba wadau na makampuni mbalimbali kupeleka huduma za kijamii pamoja na kuona wazawa wakiendelea kufanya kazi katika kambi hiyo, kazi ambazo ni za awali tu na kwamba bado kuna fursa nyingi za ajira hadi mradi utakapokamilika.

*"Watanzania changamkieni fursa zitakazotokana na ujenzi huu ili kujiongezea kipato na utaalamu kwani sehemu kubwa ya bomba linapita nchini Tanzania, Mradi huu ni wa muhimu kwa nchi yetu kwani asilimia, 80 ya bomba hili lipo upande wa Tanzania hivyo nawaomba watanzania wachangamkie fursa zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huu”* amesisitiza Dkt. Mataragio.

*Inaendelea...*

Akiwa katika makazi mapya ya mnufaika wa mradi huo, Kazimila Patrick Mshandete mkazi wa kijiji cha Sojo ambaye ni miongoni mwa wakazi zaidi 300 waliopisha maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, Dkt. Mataragio alisema Serikali imelipa fidia kwa wananchi na wengine kuwajengea nyumba za kisasa huku akibainisha kuwa taratibu zote zikiwemo za kimataifa zimezingatiwa.



"Tumefuata taratibu zote, tumewalipa fidia na kuwajengea nyumba za kisasa hivyo hakuna ukiukwaji wowote wa haki za binadamu, tunatekeleza Mradi huu kwa uwazi mkubwa na tunazingatia haki za binadamu, hakuna haki inayokiukwa", alieleza Dkt. Mataragio.



Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Kiwanda cha Kufunika mabomba katika kijiji cha Sojo, William Kajagi alisema wanaendelea na ujenzi wa msingi wa kiwanda cha kufunika mabomba kwa kutengeneza mfumo wa kuzuia joto lisipotee na hadi kufikia Mwezi Januari 2023 wanatarajia kuanza uzalishaji.

Naye mnufaika wa mradi huo, Kazimila Patrick Mshandete alisema tangu mradi wa ujenzi uanze kumekuwa na ushirikishwaji wa wanakijiji hatua kwa hatua na kwa uwazi na wananchi wameshalipwa fidia na wale waliotaka kujengewa makazi wameshajengewa nyumba za kisasa na wanapatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula kila mwezi.

# RC MTWARA AIPONGEZA TPDC KWA KASI YA USAMBAZAJI GESI ASILIA

**Tabora,**

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali  Ahmed Abbas Ahmed amelipongeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa jitihada linazozifanya hususani katika shughuli za utafiti, uendelezaji na usambazaji wa miradi ya mafuta na gesi asilia nchini.

Kanali Ahmed ameyazungumza hayo tarehe 05 Agosti, 2022 alipotembelea banda la TPDC katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kikanda Mkoani Lindi yenye kauli mbiu, ''Ajenda ya 10/30 Kilimo ni Biashara, Shiriki Kuhesabiwa kwa Mipango Bora ya Kilimo Mifungo na Uvuvi''

Akizungumza wakati huo alisema, "Naipongeza TPDC kwa kuwa imara kwenye utekelezaji wa miradi ya utafiti, uendelezaji na usambazaji wa gesi asilia nchini, vilevile naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuunga mkono miradi ya gesi asilia nchini ikiwemo mradi mkubwa wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG ) wenye thamani ya Shilingi trilioni 70 ambao utajengwa Mkoani Lindi, " alisema Ahmed.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed (Mwenye Kaunda suti ya kijivu ) akipewa maelezo ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na TPDC na Afisa Maendeleo ya Jamii wa TPDC Bw.Oscar Mwakasege mara alipowasili katika  banda la TPDC kwenye maonesho ya nane nane-Lindi

Katika hatua nyingine Afisa Maendeleo ya Jamii wa TPDC Oscar Mwakasege alieleza juu ya faida ya matumizi ya gesi asilia nchini ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa umeme ambapo 62% ya umeme nchini unazalishwa na gesi asilia, nyumba1500zimeunganishwa na gesi asilia  kwa Mkoa wa Mtwara, Lindi na Dar es salaam, magari 1400 yanayotumia gesi asilia badala ya mafuta. Katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa Mkoa wa Lindi Kata ya Mnazi mmoja nyumba 200 zitaunganishwa kutumia gesi asilia.

Mkoa wa Mtwara, Lindi na Dar es salaam, magari 1400 yanayotumia gesi asilia badala ya mafuta. Katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa Mkoa wa Lindi Kata ya Mnazi mmoja nyumba 200  zitaunganishwa kutumia gesi asilia.

Mkoa wa Mtwara, Lindi na Dar es salaam, magari 1400 yanayotumia gesi asilia badala ya mafuta. Katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa Mkoa wa Lindi Kata ya Mnazi mmoja nyumba 200  zitaunganishwa kutumia gesi asilia.

# TPDC KUJENGA BOMBA LA GESI JIPYA MTWARA



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara **Mhe. Dustan Kyobya** akizungumza na wananchi wa Kata ya Nanguruwe (moja ya Kata itakayopitiwa na bomba) katika mkutano wa uhamasishaji wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka eneo la Ntorya hadi kiwanda cha kuchakata gesi cha Madimba –Mtwara



**Mtwara,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeanza mchakato wa Ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Ntorya hadi Madimba lenye urefu wa kilomita 35.

Mchakato huo umeanza kwa kufanya mkutano wa uhamasishaji kwa wananchi wa Kata ya Madimba, Moma, Mbawala na Nanguruwe kuhusu ujenzi wa mradi huo ambao utaanzia Kijiji cha Ntorya.

Akizungumza wakati wa mkutano huo Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dustan Kyobya amesema hatua ya awali ya utafiti wa mkuza utakaotumika kupitisha bomba ulishafanyika awali na kubaini vijiji 12 vitakavyopitiwa na bomba.

Vijiji hivyo ni Namayakata, Ngorongoro, Mbawala, Mwindi, Nachenjele, Maili kumi, Ding'ida, Likweta, Minyembe, Namidondi na Mendachi.

Mhe. Kyobya alisema hatua inayokwenda kufanyika sasa ni zoezi la uthamini wa mali kwenye mkuza wa bomba wenye upana wa mita 20.

Lengo la zoezi hilo ni kutambua maendeleo yaliyofanyika katika ardhi hiyo ikiwemo nyumba, mazao na mali zingine ili kubaini thamani yake na kuandaa taratibu za malipo ya fidia kwa wamiliki watakaopisha mradi huo.

Aidha Kyobya amewataka wananchi wa maeneo ya yanayopitiwa na mradi wa bomba kutoa ushirikiano kwa TPDC wakati watakapopita kwenye maeneo yao katika zoezi uthamini.

"Naomba wananchi muwe wakweli kutoa taarifa sahihi za mmiliki wa eneo na pia muwape ushirikiano wataalamu watakaopita kwenye maeneo yenu wakati wa zoezi hilo kuepusha migogoro mbalimbali ya ardhi."

Halikadhalika, Meneja wa Biashara ya Gesi kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Mha. Emmanuel Gilbert alisema utekelezaji wa mradi huo unalenga kuongeza uzalishaji wa nishati ya gesi asilia kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia katika uzalishaji wa umeme, matumizi ya gesi kwenye magari, matumizi ya gesi viwandani pamoja na majumbani.

# UGANDA WATEMBELEA MRADI WA GESI ASILIA

Ujumbe kutoka nchini Uganda umeipongeza Serikali ya Tanzania na kufurahishwa na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi Mkoani Dar es salaam, baada ya kutembelea mradi huo.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba wakati wa ziara ya Ujumbe kutoka nchini Uganda uliohusisha Waziri wa Nchi anayeshughulikia Maendeleo ya Madini, Wizara ya Nishati na Madini nchini Uganda, Dkt. Peter Lokeris na Kamati ya Bunge ya Mazingira na Maliasili nchini humo walipotembelea Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi.

Mhandisi Mramba alisema kuwa wageni hao wameona na kufurahishwa na kazi kubwa ya uwekezaji iliyofanyika katika kutekeleza Mradi wa Kinyerezi, na kwamba wameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kutekeleza mradi huo adhimu kwa nchi za Afrika Mashariki.

Alisema ujio wao ni uthibitisho tosha kuwa nchi hizo mbili sasa ziko tayari kushirikiana katika rasilimali ya gesi asilia inayochimbwa hapa nchini.

Ujumbe wa Uganda uliwasili nchini kwa ziara ya siku sita kwa lengo la kujifunza na kuona utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya Nishati mwezi Julai, 2022 katika Mkoa wa Dar es salaam na Tanga.



# UCHAKATAJI GESI ASILIA KIVUTIO MAONESHO YA VIWANDA PWANI

**Pwani,**

Miundombinu inayoonesha mchakato wa kuzalisha, kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ilionekana kuwa kivutio kikubwa katika maonesho ya Viwanda yenye kauli mbiu "Pwani ni sehemu sahihi kwa uwekezaji, pamoja tujenge Viwanda kwa Uchumi na Ajira Endelevu" yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.



Maonesho hayo ambayo ni ya tatu kufanyika Mkoani humo yalifanyika kuanzia tarehe 05/10/2022 hadi tarehe 10/10/2022 na kuhudhuriwa na washiriki kutoka Sekta mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Pwani huku TPDC ikiwa ni miongoni mwa wadhamini katika maonesho hayo.

Aidha TPDC sambamba na kutoa elimu ya mafuta na gesi asilia kwa Wananchi na Wadau mbalimbali ambao waliweza kutembelea Banda la TPDC pia waliweza kujionea muundo wa Miundombinu ya Uchakataji wa gesi asilia.

Mgeni rasmi ambaye alikuwa Rais Mstaafu wa awamu ya nne Dkt. Jakaya Kikwete baada ya kutembelea Banda la TPDC, Mhandisi Eva Swillah alimweleza kuwa kwa sasa kuna mchato unaendelea wa kuhakikisha gesi asilia inafika Mkoani Pwani kwa sababu ya mahitaji makubwa ya matumizi ya Nishati hiyo katika Mkoa huo kutokana na ongezeko la idadi kubwa ya Viwanda.

Halikadhalika,TPDC ilipata nafasi ya kutembelea maeneo ya viwanda ambavyo vinatarajiwa kupelekewa miundombinu ya gesi asilia itakayopunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uzalishaji wa bidhaa katika viwanda hivyo mara baada ya kuanza kutumika.

Maonesho hayo pia yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa kutoka Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Mtwara, Tanga, Lindi, wenyeji Mkoa wa Pwani pamoja na wadau mbalimbali.

HABARI PICHA

# TPDC MARATHON














HABARI PICHA

# TPDC MARATHON















## VYETI KWA WADHAMINI

HABARI PICHA

# TPDC MARATHON









## VYETI KWA WADHAMINI



HABARI PICHA

# TPDC MARATHON















## ZAWADI KWA WASHINDI

# HABARI PICHA

# TPDC MARATHON















## ZAWADI KWA WASHINDI

**HABARI PICHA**

# TPDC MARATHON



















## ZAWADI KWA WASHINDI

# HABARI PICHA




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu **Balozi Ombeni Sefue** (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na timu ya TPDC iliyoshiriki Mkutano wa Africa Oil Week unaofanyika Jijini **Cape Town, Afrika Kusini.** Wengine katika picha kuanzia kulia ni **Ndg. Kelvin Komba** (Mkurugenzi wa Mkondo wa Juu TPDC), **Ndg. Paul Makanza** (Mkurugenzi wa Bodi ya TPDC), **Bi. Venosa Ngowi** (Meneja Utafutaji TPDC) na **Dkt. Wellington Hudson** (Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi TPDC)






Washiriki mbalimbali wa Mkutano wa **Africa Oil Week** wakipata taarifa mbalimbali za fursa za uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi Tanzania katika banda la maonesho la TPDC.

HABARI PICHA



Wataalamu kutoka **Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)** kwa kushirikiana na **Wataalamu kutoka ofisi ya Kamishina wa Ardhi** Mkoani Mtwara wakiendelea na zoezi la uthamini wa ardhi, mazao na nyumba za wananchi watakaopisha mkuza wa bomba la gesi asilia kutoka Ntorya hadi Madimba


**Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)**
**Benjamin W. Mkapa Pensions**
**Towers, Azikiwe/Jamuhuri Street**
**S.L.P. 2774, Dar Es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255 22 2200103/4, 2200112.**
**Nukushi: +255 22 22 2200113**
**Barua pepe: info@tpdc.co.tz**
**Tovuti: www.tpdc.co.tz**

# Jarida la TPDC

TANZANIA PETROLEUM DEVELOPMENT CORPORATION

## Toleo 16

tpdctz

www.tpdc.co.tz